

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001



OFISI YA MKUU WA WILAYA,

S.L.P 02,

LUDEWA.

TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere leo Mei 30, 2022 amefanya ziara ya kikazi katika Kata ya Ludewa na kukagua mradi mkubwa wa maji ambao unatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Katika ziara hiyo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliambatana na viongozii mbalimbali Kaimu DAS Wilaya ya Ludewa Bw. Linus Malamba, Diwani wa Kata ya Ludewa Bi. Monica Mhicho

Aidha jana Mei 29, 2022 Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alifanya ziara ya kikazi katika Kata ya Luana ambapo katika ziara hiyo aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias na Diwani wa Kata hiyo Mhe. Wilbard Mwinuka.

Pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alikagua miradi ya maendeleo inayo tekelezwa katika Kata hiyo na alipo kuwa katika Kijiji cha Mbwila alitoa elimu ya Sensa ya watu na makazi pamoja na kuwasihii wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuchanja chanjo ya UVIKO 19.

Na alipo kuwa katika kijiji cha Luana na Mholo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliongea na wananchi kwa kutuma salamu za shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipatia Wilaya ya Ludewa fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, ujenzi wa vyumba vya madarasa na ujenzi wa miundombinu ya maji.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

Chrispin B.Kalinga
Afisa Habari (W) Ludewa